

فتاوى الصيام

Fataawaas-Swiyaam

[Fataawaa za Swawm]

Mwandishi:

العلامة أحمد بن يحي النجمي

´Allaamah Ahmad bin Yahyaa an-Najmiy

Tarjama:

Wanachuoni.com

01. Ni yapi masharti ya swawm? 5

02. Kuingia kwa Ramadhaan kunathibiti kupitia mtu mmoja? 5

03. Ni lini mfungaji anatakiwa kunuia swawm yake? 5

04. Ni ipi hukumu ya kula daku baada ya kuingia alfajiri? 6

05. Ni ipi hukumu ya kufunga mpaka wakati wa daku? 6

06. Ni wajibu kwa mfungaji kula daku? 6

07. Inafaa kwa mgonjwa kuacha kufunga ikiwa swawm sio nzito kwake wala haimdhuru? 7

08. Ni ipi hukumu ya kuzimia wakati wa kufunga? 7

09. Mwenye maradhi ya moyo anaweza kuacha kufunga? 7

10. Nifunge ikiwa nasafari masaa nane? 8

11. Mfungaji akate swawm akifika katika mji usiofunga? 8

12. Inafaa kwa msafiri asiyefunga kujumuisha Swalah? 8

13. Naweza kukata swawm nikisafiri 90 km kwenda kazini? 9

14. Mwanamke anaweza kuswali na kufunga damu yake ikikatika siku mbili? 9

15. Ni ipi hukumu mfungaji kula na kunywa kwa kusahau? 10

16. Ni ipi hukumu ya kutafuna ubani na tubaku wakati wa kufunga? 11

17. Je, kuvuta sigara na tubaku kunaharibu swawm? 11

18. Ni ipi hukumu ya mfungaji kutumia wanja na kujitia manukato? 11

19. Ni ipi hukumu ya kupuuza ratiba ya muda na kukata swawm kabla ya jua kuzama? 12

20. Ni ipi hukumu mfungaji kubusu? 12

21. Ni ipi hukumu ya kukata swawm kwa adhaana inayotolewa dakika tano kabla ya jua kuzama? .. 13

22. Je, maasi yanaiharibu swawm? 13

23. Je, kupiga sindano kunaharibu swawm? 13

24. Ni ipi hukumu ya sindano na kutumia vidonge? 14

25. Ni ipi hukumu ya kutumia mafuta na penesilini kwenye kidonda? 14

26. Ni ipi hukumu ya kula na kunywa kwa kudhania kuwa bado ni usiku au kukata swawm kwa kudhania kuwa jua limeshazama? 14

27. Anayefunga swawm ya Sunnah na akamjamii mkewe kwa kusahau aendelee kufunga au inamlazimu kitu? 15

28. Muadhini aadhini kwanza kisha ndio akate swawm? 15

29. Ni wajibu kukata swawm pale tu jua linapozama? 16

31. Ni ipi hukumu ya kufunga bila ya kuswali? 16

32. Ni ipi hukumu ya mwenye kufunga na haswali? 17

33. Ni ipi hukumu ya swawm ya mtu ikiwa anaswali katika Ramadhaan tu? 17

34. Ni ipi hukumu ya kukesha usiku kutwa katika michezo? 17

35. Ni ipi hukumu ya kucheza karata katika Ramadhaan? 18

36. Ni ipi hukumu ya swawm za pamoja? 19

37. Ni ipi hukumu ya mlinganizi kuita katika swalah za pamoja? 20

38. Swawm inaathirika kwa kughushi? 22

39. Unawanasihi vipi wanafunzi wanaoghushi mtihani katika Ramadhaan? 22

40. Ni ipi hukumu kutumia vidonge katika Ramadhaan ili kuzuia hedhi? 22

41. Mtu afanye nini kwa mgonjwa ambaye hakufunga kwa miaka miwili? 23

42. Akafiri vipi kwa kufanya jimaa miaka miwili iliyopita mchana wa Ramadhaan? 23

43. Mzee asiyeweza kufunga anatoa kafara vipi? 24

44. Ni kiasi gani mzee anatakiwa kuwapa masikini? 24

45. Ni wajibu kwa wasimamizi kumlishizia maiti aliyekufa kabla ya kutimiza Ramadhaan? 24

46. Tufanye nini na swawm ya msichana wetu? 25

47. Ni bora kuswali Tarawiyh na imamu au nyumbani na familia? 25

48. Je, kisimamo cha usiku ni wajibu? 26

49. Mtu afunge kwa kufuata ratiba ya muda? 26

50. Vipi mtu asiyeweza kufunga Ramadhaan anatakiwa kuwalisha masikini? 27

51. Ni ipi hukumu ya kuamka kwa ajili ya Fajr ilihali mtu yuko katika janaba? 27

52. Ni ipi hukumu ya anayekula na kunywa kwa kukusudia mchana wa Ramadhaan? 27

53. Ni lipi linalomlazimu mtu aliyepata khabari kuingia kwa Ramadhaan mida ya asubuhi? 28

54. Ni ipi hukumu ya kuoga baada ya kumwaga? 28

55. Je, madhiy yanaharibu swawm? 28

56. Je, madhiy na wadiy vinaharibu swawm? 29

57. Kupoteza damu kunaharibu swawm? 29

58. Harufu yenye kuenea inaharibu swawm? 29

01. Ni yapi masharti ya swawm?

Swali 01: Ni yapi masharti ya swawm?

Jibu: Masharti ya swawm ni mfungaji awe muislmu, mwenye jukumu juu ya matendo yake na awe ni muweza.

02. Kuingia kwa Ramadhaan kunathibiti kupitia mtu mmoja?

Swali 02: Kuingia kwa Ramadhaan kunathibiti kupitia mtu mmoja?

Jibu: Ndio. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alikubali kuingia kwa Ramadhaan kupitia ushahidi wa bedui mmoja. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema kumwambia:

"Unashuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba mimi ni Mtume wa Allaah?" Mtu yule akasema: "Ndio." Baada ya hapo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akawaamrisha watu wafunge."[1]

03. Ni lini mfungaji anatakiwa kunuia swawm yake?

Swali 03: Ni lini mfungaji anatakiwa kunuia swawm yake?

Jibu: Swawm ya faradhi ni lazima kuinuia kabla ya kuingia alfajiri ya pili. Kuhusu swawm ya Sunnah inaweza kunuiliwa wakati wowote, hata kama ni

[1] Abu Daawuud (2340), at-Tirmidhiy (691), an-Nasaa'iy (2112), Ibn Maajah (1652) na ad-Daarimiy (1692). Dhaifu kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Irwaa'-ul-Ghaliyl" (907).

baada ya kuchomoza kwa jua, kwa sharti kabla ya hapo mfungaji asiwe alikula au alikunywa. Swawm yake ni sahihi.

04. Ni ipi hukumu ya kula daku baada ya kuingia alfajiri?

Swali 04: Ni ipi hukumu ya mwenye kula daku baada ya wakati?

Jibu: Inategemea na daku ilikuliwa lini. Ikiwa limetokea baada ya wakati kwa muda mrefu basi inatakiwa kulipwa tena. Na ikiwa limetokea isiyozidi dakika tano ni lenye kusamehewa - Allaah akitaka.

Kunapoingia alfajiri ya pili ndio imeharamishwa kula na kujuzu kuswali Fajr. Ratiba ya muda haiko mia kwa mia sawa. Inaonekana kuwa ratiba ya muda imefanywa kwa ajili tu ya usalama zaidi. Iwapo mtu ataswali baada tu ya adhaana ya Fajr tunasema kuwa swalah yake si sahihi. Ni wajibu kwake kuswali tena kwa sababu ameswali kabla ya wakati kuingia.

Kwa kifupi ni kwamba anatakiwa kuiangalia hali yake. Ikiwa alikula daku baada ya muda mrefu uliyoko kwenye ratiba ya muda ni wajibu kuilipa siku hiyo.

05. Ni ipi hukumu ya kufunga mpaka wakati wa daku?

Swali 05: Ni ipi hukumu ya kufunga mpaka wakati wa daku? Je, Maswahabah walifanya hivo?

Jibu: Inajuzu kufunga mpaka wakati wakati wa daku.

06. Ni wajibu kwa mfungaji kula daku?

Swali 06: Je, ni wajibu kwa mfungaji kula daku?

Jibu: Sio wajibu. Imependekezwa kwa sababu kunaufanya mwili kuwa na nguvu[2].

07. Inafaa kwa mgonjwa kuacha kufunga ikiwa swawm sio nzito kwake wala haimdhuru?

Swali 07: Je, inafaa kwa mgonjwa kuacha kufunga ikiwa swawm sio ngumu kwake wala haimdhuru?

Jibu: Mgonjwa anatakiwa kufunga ikiwa swawm sio ngumu kwake na wala haimuathiri.

08. Ni ipi hukumu ya kuzimia wakati wa kufunga?

Swali 08: Ni ipi hukumu ya kuzimia wakati wa kufunga?

Jibu: Kuzimia kumegawanyika sehemu mbili:

1- Ikiwa kuzimia ni kwa siku moja, nusu siku au mfano wa hayo. Kuzimia huku kuna hukumu moja kama kulala.

2- Ikiwa kuzimia ni kwa muda mrefu kama mwezi mmoja au miwili[3]. Mtu kama huyu ana hukumu moja kama mwendawazimu ambaye kalamu imenyanyuliwa kwake.

09. Mwenye maradhi ya moyo anaweza kuacha kufunga?

Swali 09: Inajuzu kwa mwenye maradhi ya moyo kuacha kufunga?

[2] Tazama Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/250).

[3] Koma.

Jibu: Maradhi ya moyo yanatofautiana. Ikiwa maradhi ya moyo ni mepesi na yanakuja muda kwa mwingine, ni wajibu kufunga. Ni wajibu vilevile kuyaepuka yale mambo yanayozidisha maradhi. Ikiwa maradhi ya moyo ni mazito kwa njia ya kwamba haiwezekani kufunga au kunayazidisha maradhi, anatakiwa aache kuufunga na badala yake alishe kwa kila siku moja masikini. Akipona baada ya hapo anatakiwa kulipa masiku yaliyobaki. Ikiwa maradhi hayatarajiwi kupona hakuna kingine kinachomlazimu zaidi ya hicho.

10. Nifunge ikiwa nasafari masaa nane?

Swali 10: Allaah anapenda zichukuliwe ruhusa Zake kama anavyolipa kwa kuasiwa. Je, nifunge au nisifunge nikisafiri masaa nane kutoka Jazaan mpaka Makkah?

Jibu: Una khiyari katika hilo.

11. Mfungaji akate swawm akifika katika mji usiofunga?

Swali 11: Kuna mtu yuko katika mji wake pindi ilipoingia Ramadhaan. Baada ya hapo akasafiri kwenda katika nchi ya jirani na kukuta wakazi wa mji huo hawajaanza kufunga. Nia yake ni kubaki katika nchi hiyo zaidi ya siku nne. Je, aache kufunga?

Jibu: Akifika katika nchi hiyo iliyo jirani na akakuta kuwa hawafungi ilihali yeye amefunga, aendelee kufunga kwa kuwa atarudi katika mji wake. Aendelee kufunga. Ama ikiwa atabaki katika nchi hiyo ya jirani ana hukumu moja kama wakazi ya kuacha kufunga.

12. Inafaa kwa msafiri asiyefunga kujumuisha Swalah?

Swali 12: Nikiwa msafiri asiyefunga inajuzu kwangu kujumuisha swalah au msafiri tu ndiye anaweza kufanya hivo?

Jibu: Kujumuisha kati ya swalah mbili haikushurutishwa kufunga. Kama msafiri inajuzu kwako kuacha kufunga na kujumuisha swalah.

Maoni sahihi ni kwamba inajuzu kufunga na kuacha kufunga katika safari. Lakini lililo bora ni kuacha kufunga kwa kuwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) anapenda zichukuliwe ruhusa Zake kama anavyochukia kuasiwa[4].

13. Naweza kukata swawm nikisafiri 90 km kwenda kazini?

Swali 13: Inafaa kwangu kukata swawm ikiwa nasafiri kazini 90 km kutoka nyumbani kwangu?

Jibu: Ndio. Umbali huu unazingatiwa kuwa ni safiri. Inafaa kwako kukata swawm hata kama vyombo vya safiri leo ni rahisi na raha. Hii ni ruhusa kutoka kwa Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Ni swadaqah Allaah aliyokupeni. Hivyo basi ichukueni swadaqah yake."[5]

14. Mwanamke anaweza kuswali na kufunga damu yake ikikatika siku mbili?

Swali 14: Kuna mwanamke alizaa na damu ikaendelea siku arubaini. Kisha damu ikakatika siku mbili. Halafu ikarudi tena. Je, alitakiwa kuswali na kufunga katika siku hizi mbili?

Jibu: Asiswali na wala asifunge isipokuwa baada ya damu yake kukatika kabisa kabisa. Ni jambo linalojulikana kuwa mwishoni wa nifasi damu yake hukatika siku mbili au tatu halafu inarudi. Midhali damu yake inakwenda na

[4] Ahmad (832). Swahiyh kwa mujibu wa al-Albaaniy katika "Swahiyh-ul-Jaami´" (1886).

[5] Muslim (686).

kurudi asiswali wala asifunge. Nifasi yake itapokatika kabisa hapo ndipo anatakiwa kujitwaharisha, kuswali na kufunga.

Kujengea juu ya hili swalah yake na swalah yake si sahihi. Kama alifunga basi ni juu yake kulipa tena. Mwanamke mwenye hedhi anayejua hedhi yake hatakiwi kufanya haraka. Damu huja na kwenda. Asubiri mpaka pale atapoona vizuri umanjano.

Alama ya kutwaharika inajulikana kwa njia mbili:

1- Damu kukatika.

2- Umanjano.

Umanjano ni majimaji yanayomtoka mwanamke na ni alama juu ya kutwaharika kwake. Yakimtoka ni alama ya kutwaharika. ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) alikuwa akiwaambia wanawake:

"Msiwe na haraka mpaka muone manjano ya wazi."[6]

Hapo ndipo ataoga, ataswali, atafunga, kugusa Qur-aan na kutembelea msikiti. ´Umm ´Atwiyyah (Radhiya Allaahu ´anhaa) amesema:

"Tulikuwa hatuzingatii umanjano na uchafu baada ya kutwaharika kitu."[7]

Bi maana baada ya alama ya kutwaharika.

15. Ni ipi hukumu mfungaji kula na kunywa kwa kusahau?

Swali 15: Ni ipi hukumu iwapo mfungaji atapitikiwa na kula na kunywa kwa kusahau?

[6] al-Bukhaariy (19).

[7] Abu Daawuud (307).

Jibu: Swawm haikatiki mfungaji akipitikiwa na kula na kunywa kwa kusahau. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kula na kunywa kwa kusahau ilihali amefunga, atimize swawm yake. Hakika si mwengine ni Allaah ndiye kamilisha na kumnywesha."[8]

16. Ni ipi hukumu ya kutafuna ubani na tubaku wakati wa kufunga?

Swali 16: Ni ipi hukumu ya kutafuna ubani na tubaku wakati wa kufunga?

Jibu: Haina shaka kuwa tubaku na sigara kunaharibu swawm. Kuhusu ubani, wanachuoni wametofautiana juu yake. Baadhi wanaonelea kuwa ni wajibu au ni bora kuiepuka. Wengine wanajuzisha hilo. Ubani unaokusanya mate unatakiwa kuepukwa. Sisemi kuwa ubani unaharibu swawm, isipokuwa imechukizwa.

17. Je, kuvuta sigara na tubaku kunaharibu swawm?

Swali 17: Je, kuvuta sigara na tumbaku kunaharibu swawm?

Jibu: Ndio. Kuvuta sigara na tubaku kunaharibu swawm. Kwa sababu kuvuta sigara na tubaku vyote viwili vinampatia mtu raha. Ni vibaya vilivoje!

18. Ni ipi hukumu ya mfungaji kutumia wanja na kujitia manukato?

Swali 18: Ni ipi hukumu mfungaji kutumia wanja na kujitia manukato?

[8] al-Bukhaariy (1933) na Muslim (1155).

Jibu: Lililo bora ni kuepuka wanja kwa sababu kuna Hadiyth dhaifu juu ya hilo. Ukitumia wanja hakuchukuwi muda mrefu isipokuwa utaanza kutema makohozi. Inatokea wanja unatoa makohozi. Mishipa inanyonya wanja unatembea ndani ya mishipa.

Manukato hayana neno. Manukato yana hukumu moja kama mioshi mingine inayovutiwa pumzi kwa ndani pasi na kukusudia. Maswahabah wa kike (Radhiya Allaahu ´anhunn) walikuwa wakipika chakula na hivyo moshi ilikuwa ni vigumu kuuepuka. Hata hivyo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuwakataza hilo. Lau (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) angefanya hivo kungelikuwa kuna uzito kwa Ummah.

Kuhusu sigara, bangi na mabomba ya sigara yanaharibu swawm. Ni katika vichafu na vilevile vinamfanya mfungaji kuwa na nguvu.

19. Ni ipi hukumu ya kupuuza ratiba ya muda na kukata swawm kabla ya jua kuzama?

Swali 19: Ni ipi hukumu ya kutofuata ratiba ya muda na kukata swawm kabla ya jua kuzama?

Jibu: Ikibainika kuwa mmekata swawm kabla ya jua kuzama, basi inakulazimuni kuilipa siku hiyo. Ama ikiwa hamjahakikisha hilo swawm yenu ni sahihi.

20. Ni ipi hukumu mfungaji kubusu?

Swali 20: Ni ipi hukumu ya mfungaji kubusu?

Jibu: Mabusu ya mzee ambaye matamanio yake ni dhaifu hayaathiri maadamu hayamsababishii kushukwa. Na ikiwa atashukwa basi ni kidogo tu. Lakini kijana anayeshukwa kwa kubusu na huenda akaenda mbali kuliko hivo ni wajibu kwake asifanye hivo.

21. Ni ipi hukumu ya kukata swawm kwa adhaana inayotolewa dakika tano kabla ya jua kuzama?

Swali 21: Ni ipi hukumu ya kufungua swawm kwa adhaana inayoadhiniwa dakika tano kabla ya jua kuzama?

Jibu: Ikiwa wamefungua wakati jua bado laonekana basi ni wajibu kwao kulipa siku hiyo. Ama ikiwa jua halionekani kwa sababu ya mawingu au mfano wa hayo na mara nyingi kunaadhiniwa dakika tano kabla ambapo ima kitu katika jua kinaonekana au lote kabisa, lililo salama zaidi ni yeye kuilipa siku hiyo.

22. Je, maasi yanaiharibu swawm?

Swali 22: Je, maasi yanaharibu swawm? Ni wajibu kwa mtenda dhambi kulipa swawm tena?

Jibu: Maasi yanatofautiana. Maasi yasiyoiharibu swawm yanaipunguza thawabu zake. Lakini hata hivyo kuna maasi yanayoiharibu swawm kama punyeto, uzinzi na mfano wa hayo. Maasi kama haya yanaiharibu swawm kabisa.

23. Je, kupiga sindano kunaharibu swawm?

Swali 23: Ni ipi hukumu ya kupiga sindano mchana wa Ramadhaan? Je, kunaharibu swawm?

Jibu: Mfungaji anatakiwa kuepuka sindano kwenye mishipa. Ama sindano kwenye misuli haina neno.

24. Ni ipi hukumu ya sindano na kutumia vidonge?

Swali 24: Ni ipi hukumu ya kupiga sindano na kutumia vidonge[9]?

Jibu: Ni jambo lisilokuwa na shaka kwamba kutumia vidonge kunaharibu swawm. Hakuna mwanachuoni anayesema kinyume.

Kuhusu sindano, inaharibu pia swawm ikiwa inapigwa kwenye mishipa. Sindano kwenye misuli inahitajia kuangaliwa. Lililo salama zaidi ni kuiepuka ikiwa hakuna dharurah ya kufanya hivo.

25. Ni ipi hukumu ya kutumia mafuta na penesilini kwenye kidonda?

Swali 25: Ni ipi hukumu ya kutumia mafuta na penesilini kwenye kidonda? Vinaharibu swawm[10]?

Jibu: Mafuta na penesilini kwenye kidonda havidhuru kwa kuwa havifiki mwilini.

26. Ni ipi hukumu ya kula na kunywa kwa kudhania kuwa bado ni usiku au kukata swawm kwa kudhania kuwa jua limeshazama?

Swali 26: Ni ipi hukumu ya kula na kunywa kwa kudhania kuwa bado ni usiku au kukata swawm kwa kudhania kuwa jua lishazama?

Jibu: Akila na kunywa huku akiwa na shaka kama alfajiri imeshaingia, swawm yake ni sahihi. Hahitajii kuilipa siku hii. Ama ikimbainikia kuwa alikula au kunywa baada ya alfajiri kuwa wazi mbali na mashaka yote, ni

[9] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/249).

[10] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/250).

lazima kwake kulipa. Hali kadhalika ikiwa alikata swawm kwa kudhania kuwa jua limeshazama. Ikimbainikia kuwa bado halijazama basi inamlazimu kuilipa siku hiyo.

27. Anayefunga swawm ya Sunnah na akamjamii mkewe kwa kusahau aendelee kufunga au inamlazimu kitu?

Swali 27: Mtu mwenye kufunga swawm ya Sunnah na akamjamii mke wake kwa kusahau aendelee kufunga au inamlazimu kitu?

Jibu: Kitendo cha kusahau inapokuja katika jamii kiko mbali. Kwa sababu jimaa ni jambo la kushirikiana baina ya mwanaume na mwanamke. Mmoja katika wanandoa akisahau mwingine atamkumbusha. Jimaa inahitajia kufunga milango na mambo mengine yanayopingana na kusahau.

28. Muadhini aadhini kwanza kisha ndio akate swawm?

Swali 28: Sisi tuna muadhini ambaye watu wanamfuata katika adhaana ya Maghrib. Anaadhini pale tu jua linapozama. Je, akate swawm kwanza kisha ndio aadhini? Au anatakiwa aadhini kwanza kisha ndio akate swawm kwa kuzingatia kuwa watu wanamfuata yeye[11]?

Jibu: Yote mawili yanajuzu. Akiwa na uhakika kuwa jua limeshazama akate swawm kwa tende na anywe maji halafu aadhini. Anaweza vilevile akaadhini kwanza kisha ndio akate swawm. Napendekeza hili la pili.

[11] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/252).

29. Ni wajibu kukata swawm pale tu jua linapozama?

Swali 29: Ni wajibu kwa mfungaji kukata swawm pale tu jua linapozama[12]?

Jibu: Sio wajibu. Imependekezwa kwa kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema pindi alipokataza kuunganisha swawm:

"Anayetaka kuendelea na swawm basi aendelee mpaka wakati wa daku."[13]

30. Ni ipi hukumu ya kufunga alhamisi kisha ijumaa?

Swali 30: Nilifunga siku ya alhamisi na ijumaa. Inajuzu?

Jibu: Ndio.

31. Ni ipi hukumu ya kufunga bila ya kuswali?

Swali 31: Ni ipi hukumu ya kufunga bila ya kuswali?

Jibu: Hivi kweli inawezekana kufunga bila ya kuswali? Kufanya nguzo ya nne na kuacha nguzo ya pili? Mtu awe muislamu kunahitajia kukubali uwajibu wa swawm na wa hajj tofauti na swalah. Haitoshi kukubali uwajibu wake tu. Asiyeswali ni wajibu kumtaka atubie. Ima atubie au auawe hali ya kuwa ni kafiri. Haya ndio maoni sahihi ilihali wanachuoni wengi wanasema kuwa auawe hali ya kuwa ni mtenda dhambi.

Wale wasiomkufuruisha asiyeswali wanasema atauawa hali ya kuwa ni mtenda dhambi. Dalili zinafahamisha kuwa asiyeswali ni kafiri ambaye damu na mali yake ni halali. Ikisihi kama kweli anaacha swalah kwa kukusudia, ni mwenye kuritadi. Katika hali hiyo anatakiwa kuwekwa mbele ya hakimu wa Kishari´ah na amtake kutubia. Ima atubie au amhukumu kifo kikafiri.

[12] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/250).

[13] ad-Daarimiy (1705).

Tukisema kuwa ni kafiri basi hatutotakiwa kumtembelea pindi atapokuwa mgonjwa wala kumswalia pindi atapokufa. Mali yake itakuwa ni fai ya waislamu. Asiwarithi warithi wake na wala wao wasimrithi. Aidha mke wake anatengana na yeye moja kwa moja. Hukumu zote hizi anatakiwa kutekelezewa.

32. Ni ipi hukumu ya mwenye kufunga na haswali?

Swali 32: Ni ipi hukumu ya mwenye kufunga ilihali haswali?

Jibu: Swawm yake si sahihi ikiwa haswali. Allaah akimwongoza atamsamehe. Tawbah inafuta ya kabla yake.

33. Ni ipi hukumu ya swawm ya mtu ikiwa anaswali katika Ramadhaan tu?

Swali 33: Kuna mtu haswali isipokuwa Ramadhaan tu. Ni ipi hukumu ya swawm yake?

Jibu: Huyu ni kama vile hakuswali wala hakufunga.

34. Ni ipi hukumu ya kukesha usiku kutwa katika michezo?

Swali 34: Ni ipi hukumu ya kukesha usiku wa Ramadhaan na kucheza?

Jibu: Ni kupoteza wakati. ´Ibaadah ni mtu kuutumia usiku kwa kuswali, kusoma Qur-aan na kusoma elimu. Watu hawa wanapoteza usiku katika mipira na michezo. Hii bila ya shaka ni kupoteza wakati. Kisha wanautumia mchana kutwa na wanaamka karibu na kuzama kwa jua. Huenda hawaswali Fajr, Dhuhr na ´Aswr. Hii ni dhambi kubwa!

35. Ni ipi hukumu ya kucheza karata katika Ramadhaan?

Swali 35: Ni ipi hukumu ya kucheza karata katika Ramadhaan?

Jibu: Kujishughulisha na mambo ya upuuzi ni haramu mbali na Ramadhaan na ni khatari zaidi katika Ramadhaan. Mwenye kunyimwa fadhila za mwezi huu hakika huyo ni mkhasirikaji mkubwa. Wenye kutumia nyusiku zao katika kucheza karata na mfano wa upotezaji muda mwingine kama televisheni ni mwenye kunyimwa kheri nyingi. Je, kusoma Qur-aan, kuswali swalah za Sunnah, kutafuta elimu na kukaa na watu wema hakutoshelezi? Watu hawa wanatakiwa wamche Allaah.

Mabarobaro wanaotoka na kucheza kuanzia 20:00 mpaka 04:00 wanatumia masaa nane katika michezo. Wanajiweka wenyewe katika madhambi na maneno mabaya. Huu ni upuuzi mbaya.

Jambo la pili sisi wote tuna majukumu kwa wale walio chini yetu. Baba mwenye kutoka nyumbani na kuwaacha watoto wake wanalala ni mwenye jukumu kwao. Ni wajibu kwake kuwafanyisha mazoezi watoto wake katika kumtii Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala), kuwaamsha katika swalah, kuwafanya watende matendo mema na kuwafunza ukomavu. Huenda Allaah akamnufaisha kwa hilo.

Tukiwaacha watoto wakatoka na kwenda watakapo na wakarudi nyumbani pasi na kuswali, haina shaka kwamba yule mkubwa ndiye mwenye kubeba majukumu makubwa kwa hilo. Yule mkubwa anatakiwa kumcha Allaah juu ya wale walio chini yake. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amesema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا قُوا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا

"Enyi mlioamini! Zikingeni nafsi zenu na ahli zenu kutokamana na Moto." (66:06)

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Nyote ni wachungaji na nyote mtaulizwa juu ya kile mlichokichunga. Mwanaume ni mchungaji kwa familia yake na ataulizwa juu yao. Mwanamke ni mchungaji na ataulizwa juu ya nyumba ya mumewe."[14]

Sisi wakubwa iwapo tutaapuuza wachungwa wetu na tukaacha majukumu yetu, basi Allaah atatuuliza juu ya hilo. Hakika sisi tunaogopa adhabu ya Allaah (´Azza wa Jall).

Jambo la tatu tunatakiwa kusadiana katika wema na uchaji Allaah. Ukimuona mtu watoto wake wanaenda vibaya, anawapuuza na hawafunzi, hawaamrishi mema na kuwakataza maovu, basi unalazimika kumzindua juu ya hilo. Haya ndio wayawezayo. Wanaweza kuzungumza, kunasihi na kuwaelekeza waja wa Allaah.

36. Ni ipi hukumu ya swawm za pamoja?

Swali 36: Ni ipi hukumu ya swawm za pamoja, swalah za pamoja na ´ibaadah kama hizo?

Jibu: Hii ni katika madhambi mazito. Sisi tunawajua watu hawa ambao wanawawajibishia watu mambo ambayo Allaah hakuwawajibishia. Wanafanya hivo kwa njia ya kutaka kupendezesha na wanaita kuwa ni "swalah za pamoja" na mengineyo. Sisi tunawajua watu hawa na tunazijua hali zao zilivyo. Watu wote wanawafahamu. Kitendo hichi ni batili. Mwenye kuamrisha hilo amejifanya mwenyewe kuwa ni muweka Shari´ah pamoja na Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na amewajibisha kitu ambacho hakikuwajibishwa na Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) mwenyewe hakumuamrisha mtu kusimama usiku wala kufunga baadhi ya siku.

[14] al-Bukhaariy (7138) na Muslim (1829).

Watu hawa ni juu yao kumcha Allaah na kutubia kwa yale wanayoita "swawm za pamoja", "swalah za pamoja" na mfano wa hayo. Haijuzu kabisa. Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amesema:

أَمْ لَهُمْ شُرَكَاءُ شَرَعُوا لَهُم مِّنَ الدِّينِ مَا لَمْ يَأْذَن بِهِ اللَّهُ ۚ وَلَوْلَا كَلِمَةُ الْفَصْلِ لَقُضِيَ بَيْنَهُمْ ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

"Je, wanao washirika waliowaamuru dini yale ambayo Allaah hakuyaidhinisha? Kama si neno la uamuzi, ingelikidhiwa baina yao - na hakika madhalimu watapata adhabu yenye kuumiza." (42:21)

37. Ni ipi hukumu ya mlinganizi kuita katika swalah za pamoja?

Swali 37: Kuna vijana wanaotaka kuwalingania watu katika dini ya Allaah na kuwalea vijana juu ya Uislamu. Wanatumia baadhi ya barnamiji kama swalah za pamoja katika baadhi ya siku. Ni ipi hukumu ya kitendo chao[15]?

Jibu: Da´wah inatakiwa iwe juu ya Sunnah za Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Haikupokelewa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwaambia Maswahabah wake (Radhiya Allaahu ´anhum):

"Tuache tufunge siku moja swawm ya Sunnah ya pamoja."

Kitu kilichopokelewa tu ni kuwa Salamah bin al-Akwa´ (Radhiya Allaahu ´anh) ameeleza kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimwamrisha mwenye kusilimu akiri kati ya watu:

"Mwenye kufunga atimize swawm yake. Aliyekula asile kitu zaidi na badala yake atimize swawm yake."[16]

Katika upokezi mwingine ar-Rubayy´ bin Mu´awwidh bin ´Afrah ameeleza:

[15] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/252).

[16] Ahmad (16508).

"Asubuhi ya ´Aashuuraa´ Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alituma mjumbe kwenda katika vijiji vya Aswaar nje ya al-Madiynah akisema: "Aliyeamka asubuhi hali ya kuwa amefunga basi atimize swawm yake. Aliyeamka asubuhi hali ya kuwa hakufunga basi atimize siku yake iliyobaki."[17]

Mwanzoni mwa Uislamu, kabla ya Ramadhaan kuwa faradhi, ilikuwa ni wajibu kufunga ´Aashuuraa´. Anayetaka kuwafunza mabarobaro haifai akamkalifisha yeyote kufunga swawm ya pamoja. Ni Bid´ah ikiwa malengo ni kumuabudu Allaah. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Mwenye kuzua katika amri yetu hii yasiyokuwemo atarudishiwa mwenyewe."[18]

Badala yake mlinganizi anatakiwa kuwabainishia wanafunzi wake fadhila za swawm na fadhila zinazopatikana katika kufunga jumatatu na alhamisi, masiku meupe au siku tatu katika Ramadhaan. Asimwamrishe yeyote kufunga siku maalum. Awaache watu wafunge wao wenyewe kwa kutaka kwao. Akiwaamrisha kufunga basi amefanya lililopendekezwa kwenda katika faradhi. Ni uwekaji Shari´ah ambao haukuidhinishwa na Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hukumu zinatakiwa ziwe kama zilivyo na kama zilivyokuwa pindi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipokufa. Mlinganizi anatakiwa tu kubainisha na kutaja zile Hadiyth zinazovutia katika matendo mema bila ya kuwalazimisha kitu. Kama jinsi tunawajibika kumuiga Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kizazi chake katika mambo yote, kadhalika tunawajibika kumfuata Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) pindi tunapoita katika dini ya Allaah (Tabaarak wa Ta´ala).

[17] Muslim (1919).

[18] al-Bukhaariy (2697) na Muslim (1718).

38. Swawm inaathirika kwa kughushi?

Swali 38: Inatokea wakati mwingine baadhi ya wanafunzi wanaghushi katika mchana wa Ramadhaan. Je, kughushi kunaathiri swawm zao?

Jibu: Kughushi ni kitu kimoja na swawm ni kitu kingine.

39. Unawanasihi vipi wanafunzi wanaoghushi mtihani katika Ramadhaan?

Swali 39: Tunataka uwape nasaha vijana wanaoghushi mtihani katika Ramadhaan?

Jibu: Wanafunzi wamenishinda na hawasikilizi maneno yangu. Wakati nilipokuwa nikiwachunga katika mtihani nilikuwa nawakumbusha maneno ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam):

"Mwenye kujipamba kwa kitu asichokuwa nacho ni kama mtu aliyevaa nguo mbili za uongo."[19]

Ni juu yako kutosheka na elimu uliyopewa na Allaah. Inakutosha kutatua matatizo.

40. Ni ipi hukumu kutumia vidonge katika Ramadhaan ili kuzuia hedhi?

Swali 40: Ni ipi hukumu ya kutumia vidonge vya kuzuia hedhi katika Ramadhaan tu kwa lengo la kufunga mwezi mzima?

Jibu: Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amewaruhusu wanawake kutofunga wakati wa hedhi na nifasi. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

[19] al-Bukhaariy (5219) na Muslim (2129).

"Sijapata kuwaona wapungufu wa akili na dini kama nyie, mwanaume mwenye busara anaweza kupotoshwa na mmoja wenu." Wakauliza: "Ni upi upungufu wa dini na akili yetu?" Akasema: "Kuhusu upungufu wa akili yake, Allaah amefanya ushahidi wa wanawake wawili ni sawa na ushahidi wa mwanaume mmoja. Ama upungufu wa dini yake, anapokuwa na hedhi hafungi na wala hawaswali."[20]

Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) amemruhusu mwanamke kutofunga kipindi yuko na hedhi na nifasi. Hahitajii kutumia vidonge ili kufunga mwezi mzima. Isitoshe ni kwamba vidonge hivi vinawaathiri wanawake ndio maana wanatakiwa kuviepuka.

41. Mtu afanye nini kwa mgonjwa ambaye hakufunga kwa miaka miwili?

Swali 41: Kuna mgonjwa mmoja ambaye hakufunga kwa miaka miwili. Je, alishiziwe au afungiwe?

Jibu: Alishiziwe.

42. Akafiri vipi kwa kufanya jimaa miaka miwili iliyopita mchana wa Ramadhaan?

Swali 42: Miaka sita iliyopita kuna mtu alimjamii mke wake mchana wa Ramadhaan. Mpaka sasa hajatoa kafara. Ni lipi la wajibu kwake?

Jibu: Inategemea na hali yake. Haijuzu kwake kuchelewesha kafara. Ni wajibu kwake kutoa kafara. Ikiwa hawezi kufunga miezi miwili mfululizo, atoe kafara kwa kuwalisha masikini. Ikiwa anaweza kufunga basi ni lazima atoe kafara kwa kufunga.

[20] al-Bukhaariy (304) na Muslim (80).

43. Mzee asiyeweza kufunga anatoa kafara vipi?

Swali 43: Kuna mtu ni mzee na hawezi kufunga. Je, alishe maskini mmoja kwa kila siku moja au alishe masikini sitini katika mwezi?

Jibu: Alishe masikini mmoja kwa kila siku moja.

Atatakiwa kulisha masikini sitini pindi ataposema kuwa mgongo wa mke wake kwake ni kama mgongo wa mama yake (*Dhwihaar*). Haihusiani na kulisha katika Ramadhaan.

Lililo salama zaidi ni yeye alishe masikini kumi kukipita siku kumi za Ramadhaan, halafu alishe masikini kumi wengine kukipita siku kumi za Ramadhaan kisha alishe masikini kumi wengine mwishoni mwa Ramadhaan.

44. Ni kiasi gani mzee anatakiwa kuwapa masikini?

Swali 44: Mzee asipoweza kufunga badala yake anawalishiza masikini chakula kama inavyojulikana. Chakula hichi kinatakiwa kupima kiwango gani? Inafaa kuwalishiza chakula masikini kwa kuwapa chakula cha mchana na cha jioni?

Jibu: Chakula kinatakiwa kiwe Mudd. Mudd ni sawa na gramu 600. Kwa ajili hiyo tunawaambia watu katika nchi hii watoe 1 kg kwa kuzingatia ya kwamba watu katika nchi hii wako katika hali nzuri na himdi zote zinamstahikia Allaah. Vinginevyo ni kuwa kiwango cha wajibu ni chini ya 1 kg.

45. Ni wajibu kwa wasimamizi kumlishizia maiti aliyekufa kabla ya kutimiza Ramadhaan?

Swali 45: Kuna mtu asiyeweza kufunga amekufa kabla ya Ramadhaan kwisha. Je, ni wajibu kwa wasimamizi wake kumlishizia?

Jibu: Sio wajibu kwa wasimamizi wake kumlishizia.

46. Tufanye nini na swawm ya msichana wetu?

Swali 46: Nina msichana wangu aliyefariki mwezi uliyopita. Ana siku sita zinazomlazimu za Ramadhaan. Ni lipi linalotulazimu juu ya swawm hiyo? Je, tumfungie, tumtolee swadaqah au hakuna linalotulazimu[21]?

Jibu: Ikiwa msichana wenu alikuwa anaweza kulipa lakini hamkulipa, basi hapo mtakuwa na wajibu wa kumfungia au kumlishizia kwa kila siku moja ambayo hakufunga. Ikiwa mtachagua hilo la pili mtatoa 1 kg mchele au ngano. Ama ikiwa maradhi yake yaliendelea mpaka akafariki si nyinyi wala yeye haimlazimu kitu.

47. Ni bora kuswali Tarawiyh na imamu au nyumbani na familia?

Swali 47: Ni lipi lililo bora mtu aswali Tarawiyh pamoja na imamu au nyumbani pamoja na familia kwa kuwa wanafamilia hawajui kusoma Qur-aan?

Jibu: Hapana shaka kwamba kuswali nyumbani na kuswali na familia ndio bora zaidi. Inafaa vilevile akaswali na imamu kisha akarudi nyumbani kabla ya Witr kuswali na familia. Hakuna neno lau ataswali zaidi ya Rakaa´ kumi au kumi na tatu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuweka kiwango maalum cha Rakaa´. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aliswali Rakaa´ kumi na moja au kumi na tatu bila ya kuweka kiwango cha Rakaa´ maalum. Alimwambia (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ´Abdullaah bin ´Amr (Radhiya Allaahu ´anhumaa):

"Nimepata khabari kwamba unaswali usiku mzima na wala hulali na unafunga mchana." ´Abdullaah akasema: "Ndio, nafanya hivo." Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam)

[21] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/252).

akamwambia: "Usifanye hivo. Ukifanya hivo basi nafsi yako itachoka na macho yako yadhoofika. Nafsi yako kwako ina haki, familia yako kwako ina haki na mke wako kwako na haki. Kwa hiyo mpe kila mmoja haki yake."[22]

Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hakuweka kiwango cha Rakaa´ maalum. Pindi mwanamke alipomjia ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) na kumueleza kuhusu swalah yake Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alimwambia:

"Fanyeni kile mnachoweza. Hakika Allaah hachoki mpaka nyinyi mchoke."[23]

48. Je, kisimamo cha usiku ni wajibu?

Swali 48: Je, kisimamo cha usiku ni wajibu?

Jibu: Kisimamo cha usiku sio wajibu. Ni kitu tumewekwa katika Shari´ah. Swawm ni faradhi na kisimamo cha usiku ni Sunnah.

49. Mtu afunge kwa kufuata ratiba ya muda?

Swali 49: Je, mtu afuate ratiba ya muda inapokuja katika kuanza na kukata swawm katika Ramadhaan?

Jibu: Kwa hali yoyote anatakiwa kuzingatia kupambazuka na kuzama kwa jua. Hilo ndilo lililo salama zaidi. Ratiba ya muda inayoonesha kuamrisha swawm kabla ya kupambazuka ni jambo la usalama kwa uhakika.

[22] al-Bukhaariy (1979) na Muslim (1159).

[23] Muslim (782).

50. Vipi mtu asiyeweza kufunga Ramadhaan anatakiwa kuwalisha masikini?

Swali 50: Mtu asiyeweza kufunga Ramadhaan awalishe masikini vipi?

Jibu: Asiyeweza kufunga baada ya kupita siku kumi za Ramadhaan anunue 10 kg za mchele mzuri na aipe familia ya kifakiri. Siku zingine ishirini za Ramadhaan zikipita anafanya hali kadhalika. Pindi Ramadhaan inaisha kabisa afanye vivyo hivyo.

51. Ni ipi hukumu ya kuamka kwa ajili ya Fajr ilihali mtu yuko katika janaba?

Swali 51: Ni ipi hukumu ya kulala katika hali ya janaba na kukaadhiniwa kwa ajili ya swalah ya Fajr ilihali mtu yuko katika hali hiyo hiyo?

Jibu: Swawm yake ni sahihi na ni wajibu kwake kuoga.

52. Ni ipi hukumu ya anayekula na kunywa kwa kukusudia mchana wa Ramadhaan?

Swali 52: Ni ipi hukumu ya mwenye kula na kunywa katika mchana wa Ramadhaan ilihali yuko na afya njema? Ni lipi linalomlazimu?

Jibu: Haijuzu kwa mtu kula na kunywa katika mchana wa Ramadhaan ilihali yuko na afya njema. Ni wajibu kwake kujizuia na kula na kunywa na ni wajibu kwake kulipa siku hiyo.

53. Ni lipi linalomlazimu mtu aliyepata khabari kuingia kwa Ramadhaan mida ya asubuhi?

Swali 53: Kuna mtu Ramadhaan imeingia na akaja kupata khabari mida ya asubuhi. Ni lipi linalomlazimu?

Jibu: Baada ya kupata khabari kuwa ni Ramadhaan ni wajibu kwake kujizuia na kula na kunywa na kuilipa siku hiyo.

54. Ni ipi hukumu ya kuoga baada ya kumwaga?

Swali 54: Wanachuoni wametofautiana juu ya uwajibu wa kuoga baada ya kumwaga. Nini hukumu ya hilo?

Jibu: Ni wajibu kuoga baada ya kumwaga. Pindi mtu anapomwaga basi ni wajibu aoge. Lakini akiota bila ya kumwaga hakuna kinachomlazimu. Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

"Maji yanatokamana na maji."

Hadiyth imefutwa kwa upande mmoja na hukumu yake ni yenye kubaki kwa upande mwingine. Imefutwa kutokana na jimaa. Ni wajibu kuoga baada ya jimaa hata kama mtu hakumwaga. Dhakari ikiingia tu ndani ya tupu inakuwa ni wajibu kuoga.

Kuhusu ndoto za kimapenzi, ni wajibu kuoga pale tu ambapo mtu atamwaga. Endapo hatomwaga, basi sio wajibu kwake kuoga.

55. Je, madhiy yanaharibu swawm?

Swali 55: Kuna mtu amecheza na mke wake mchana wa Ramadhaan ilihali amefunga ambapo akatokwa na madhiy. Je, swawm yake ni sahihi? Hakumjamii.

Jibu: Kutokwa na madhiy hakuharibu swawm. Kinachoharibu swawm ni manii. Mwanaume au mwanamke akitokwa na manii ni wajibu kuilipa siku hiyo. Madhiy ni yenye kuwapata wanaume na wanawake na kwa ajili hiyo hatuwezi kusema kuwa ni wajibu kwao kuilipa siku hiyo.

56. Je, madhiy na wadiy vinaharibu swawm?

Swali 56: Je, madhiy[24] na wadiy[25] vinaharibu swawm?

Jibu: Hapana.

57. Kupoteza damu kunaharibu swawm?

Swali 57: Kuna mtu alikanyaga msumari kazini kwake na damu ikaanza kutoka kwenye mguu wake. Je, hili linaharibu swawm?

Jibu: Haliharibu swawm. Kubwa linaloweza kusemwa ni kwamba mwili wa mfungaji unadhoofika ikiwa damu yenye kutoka ni nyingi.

58. Harufu yenye kuenea inaharibu swawm?

Swali 58: Harufu yenye kuenea, kama petroli, inaharibu swawm[26]?

Jibu: Hapana, haiharibu swawm isipokuwa ikiwa kama mtu atanusa kwa kukusudia.

---

[24] Ni majimaji yanayofanana na manii yanayotoka kwenye tupu ya mbele kwa sababu ya kucheza na kumwangalia mwanamke.

[25] Ni maji meupe mepesi yanayotoka baada ya kukojoa au wakati wa kubeba kitu kizito.

[26] Kutoka "Fath-ur-Rabb al-Waduud" (1/251).

Mwisho